Mwongozo Wa Mwalimu

2

Kuitazama Biblia Kwa Haraka

Kutambulisha neno la Mungu

MVMM

Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

Kuitazama Biblia Kwa Haraka

Kutambulisha neno la Mungu

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwalimu

Toleo la Tano

MVMM
Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

Kuitazama Biblia Kwa Haraka

Kutambulisha neno la Mungu

Kimeandikwa Na David Batty
Mwongozo Wa Mwalimu
Toleo la tano

Maandiko Yanayotumiwa Katika Kitabu Hiki Yametoka Kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2023, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii yaKiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwa mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo:
A Quick Look at the Bible, 5th edition

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* yanatawaliwa ili kutumiwa makanisani, shuleni, katika huduma za gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vilevile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, cha Mwongozo Wa Somo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.orgna
www.iTeenChallenge.org

MVMM
Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 02-2023

Kuitazama Biblia Kwa Haraka

Somo hili linatoa utangulizi wa jumla kuhusu Biblia nzima. Wazo moja kubwa tunalotaka kufikisha kwa wahusika kupitia somo hili ni kwamba, Biblia ni kitabu maalum – ni kitabu cha Mungu. Unaweza kuiamini. Ni ya kweli. Ujumbe wake hautabadilika.

1

Sura Ya 1. Habari za jumla kuhusu Biblia

Sehemu hii inahusu habari kama, vitabu ni vingapi, waandishi, na ni lini kiliandikwa. Pia tunazungumzia jinsi Kristo anavyohusika katika Biblia nzima.

2

Sura Ya 2. Jinsi Biblia ilivyoandikwa

Hili somo linatazama maana ya "uvuvio". Mungu aliwavuviaje watu waandike Biblia? Pia tunapata kugundua jinsi Biblia ilivyoandikwa, na jinsi ambavyo imepita katika vizazi vingi hadi kutufikia sisi leo hii.

3

Sura Ya 3. Nawezaje kujua kwamba Biblia ni sahihi?

Sura hii inatoa nafasi ya kutafiti ushahidi wenye kuthibitisha kwamba Biblia ni ya kweli.

4

Sura Ya 4. Kulitazama Agano la Kale kwa kifupi

Pamoja na kufanya mapitio mafupi ya Agano la Kale, tunatumia pia kijitabu cha David Fant kiitwacho (tafsiri), ***Ijue Biblia Yako***, kinachotoa muhtasari mfupi kwa kila kitabu katika Biblia.

5

Sura Ya 5. Kulitazama Agano Jipya kwa kifupi

Mkazo maalum unawekwa kwenye maisha ya Yesu na kusudi la unabii.

Yaliyomo Katika Mwongozo Huu Wa Mwalimu

Kitabu hiki kina sehemu nne. Kila sehemu imeanza kwa ukurasa wenye rangi ya njano, ambao ni ukurasa ulio na jina la mada.

1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo
2. Mwongozo Wa Mwanafunzi
3. Mwongozo Wa Somo
4. Mtihani Wa Mwanafunzi Na Cheti Cha Somo

Maelezo kuhusu jinsi ya kutumia kila sehemu yanapatikana mara tu baada ya utangulizi wa ukurasa unaofuata.

Utangulizi

Hili ni somo moja katika mfululizo wa masomo ulioandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha Wakristo wapya. Tunaamini kwamba lipo hitaji kubwa sana siku hizi la kuwasaidia Wakristo wapya ili wahusishe mafundisho ya Kristo na maisha yao ya kila siku kwa vitendo. Mafundisho haya pia yanaweza kutumiwa vizuri sana kwa ajili ya huduma kwa vijana kanisani na watu wazima wanaotamani kufanya Ukristo kuwa sehemu ya maisha yao kila siku.

Kusudi kubwa la somo hili na mfululizo mzima wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* ni kuwatambulisha Wakristo wapya kwa maswali muhimu yanayohusu maisha. Hatujaribu kuwapa mafundisho yatakayokuwa ndiyo mwisho kuhusu mada husika.

Kamati ya Mtaala ya Huduma ya Teen Challenge Marekani, ina mpango wa kuendelea kupitia upya na kufanya marekebisho kwa masomo haya. Tunakaribisha mawazo yoyote au hoja za kutusaidia kuyaboresha.

Jinsi ya kutumia Mwongozo huu Wa Mwalimu

1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo

Kurasa za kwanza katika sehemu hii zinatoa mtazamo wa somo zima kwa ufupi.

Ukurasa unaofuata utakuwa ni nakala ya ***Orodha Ya Kazi Za Darasani***. Hii orodha inaonyesha wakati ambapo kila zoezi katika Mwongozo wa Somo linatakiwa kukamilishwa, na wakati kila chemsha bongo na mtihani zitatolewa. Kila mwanafunzi anapaswa kupewa habari stahiki kwa ajili ya ukurasa huo mwanzoni mwa kila somo. Kitabu hiki cha Mwongozo wa Somo tayari kina nakala isiyoandikwa chochote ya fomu hiyo, kwenye jalada la nyuma upande wa ndani.

Kitakachofuata ni mipango kwa ajili ya kufundishia kila somo. Hiyo yote ina kitu kinachoitwa Kweli Kuu ya Kibiblia pamoja na Mstari Mkuu. Hivyo vitu viwili vinaweza kutolewa mwanzoni mwa kipindi cha darasa. Pia vinasaidia kufanya mjadala ulenge yanayotakiwa kwa wakati wote.

Chini ya Kweli Kuu ya Kibiblia na Mstari Mkuu, kuna maelezo machache jinsi ya kufundisha somo lenyewe. Mara nyingi, marejeo yanaelekezwa kwa Mwongozo wa Mwanafunzi au kwa Zoezi linalopatikana katika Mwongozo wa Somo.

Kila somo humalizika kwa shughuli ya kufanya katika “Kufanyia Kazi Somo Maishani.” Umuhimu wa kipengele hiki hauelezeki. Wakristo wapya wanahitaji mwongozo ulio wazi kuhusu jinsi ya kuanza kufanyia kazi mafundisho haya katika maisha yao ya kila siku. Hakikisha kwamba una toa nafasi ya kutosha ili kuwasaidia wanafunzi wako kuanzisha shughuli hii.

Mwisho wa kila mpango wa kufundishia somo kuna orodha ya kazi za wanafunzi kufanya.

Mengi katika masomo haya yalikusudiwa kuwa na vipindi vitano vya darasa, kila kimoja kikidumu kwa saa moja. Kipindi cha mwisho darasani ni kwa ajili ya mtihani. Masomo yote 14 katika mfululizo huu yanaweza kukamilishwa katika kipindi cha miezi kati ya mitatu hadi

minne, kama darasa litakutana kwa siku tano katika wiki. Ikiwa unafanya darasa kwa saa moja tu kwa juma, unaweza kukamilisha somo moja kwa mwezi – na mfululizo wote kwa kama mwaka mmoja. Mengi katika haya masomo yanaweza kupanuliwa na kufundishwa kwa muda mrefu, au kwa madarasa zaidi.

2. Mwongozo Wa Mwanafunzi

Kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwanafunzi chaweza kutimiza makusudi mawili. Unaweza kutaka wanafunzi wasome kurasa husika katika kujiandaa kwa ajili ya somo linalofuata. Au, unaweza kuwataka wakisome baada ya wewe kufundisha somo, ili kufanya kama marudio na kuwa kama njia ya kusisitiza na kukazia kilichofundishwa darasani.

Tunakutia moyo uwaambie wanafunzi wajiandikie notsi darasani, hata ingawa utawapa Mwongozo Wa Mwanafunzi. Wanayojiandikia wenyewe pamoja na mazungumzo na mijadala darasani vitawasaidia sana kuelewa vizuri baadhi ya mada zinazoshughulikiwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

3. Mwongozo Wa Somo

Mazoezi yaliyo katika Mwongozo wa Somo yameandaliwa ili kumpa mwanafunzi kazi ya kufanya nje ya darasa. Baadhi ya kazi-mradi hizo zinasaidia kumwandaa mwanafunzi kwa ajili ya somo la darasa linalofuata.

Mengi ya mazoezi haya yamekusudiwa kuwasaidia wanafunzi wajikite ndani zaidi na kutazama baadhi ya maswala yanayojadiliwa darasani kwa kina. Lengo kuu la kazi hizo nyingi ni kuwaasaidia wanafunzi wagundue njia za kufanyia kazi hizo za kweli za Biblia katika maisha yao ya kila siku.

4. Mtihani Wa Mwanafunzi na Funguo la Majibu ya Mtihani

Mitihani hii imeandaliwa ili kutoa kipimo rahisi tu cha maendeleo ambayo kila mwanafunzi alipata katika uelewa wa kweli za Biblia zinazoshughulikiwa katika somo hili. Karatasi ya Majibu kwa ajili ya mtihani husika iko mara tu baada ya ukurasa wa mwisho wa ile nakala mfano ya mtihani wa mwanafunzi, katika Mwongozo huu wa Mwalimu.

5. Cheti Cha Somo

Cheti cha somo ni kwa ajili ya kuwatambua wale wanaomaliza kazi yote inayotakiwa kwa ajili ya somo hili na kufaulu mtihani. Mfano wa cheti hicho cha somo upo katika ukurasa wa mwisho wa kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwalimu. Cheti cha Kufuzu pia kinapatikana kwa wale wanafunzi wanaomaliza masomo yote 14 katika mfululizo huu wa *Mafunzo ya Vikundi Ya Maisha Mapya*. Pia, mfano upo katika kile kitabu kinachoitwa ***Kuwatambulisha waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***.

Jinsi Masomo Haya Yalivyotokea

Sulemani alisema, hakuna kitu kipya chini ya jua. Maneno hayo yanaweza kufaa hata kuhusu masomo haya. Mawazo yake mengi si mapya. Tunataka kutoa shukrani zetu maalum kwa Institute in Life Principles (Taasisi Ya Kanuni Za Maisha) kwa ushawishi mkubwa katika maisha ya watu waliotayarisha masomo haya. Masomo mengi yana alama za huduma hiyo ya Institue in Life Principles.

Nataka pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wengi sana na maelfu ya Wakristo wapya ambao wametumia masomo haya katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita. Mawazo yao yamekuwa na mchango mkubwa sana katika maandalizi ya masomo haya.
Pia ninamshukuru sana Ndugu Don Wilkerson kwa kunipa nafasi ya kufanya kazi katika kituo cha huduma ya Teen Challenge pale Brooklyn, New York, tokea mwaka wa 1971 hadi 1975. Katika miaka hiyo ndipo matayarisho yalipoanza ya masomo haya yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*.

Toleo la tano la *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* lilitayarishwa kwa msaada wa kamati ya Mitaala ya huduma ya Teen Challenge Marekani. Natoa shukrani maalum kwa wote waliosaidia katika mapitio na marekebisho hayo.

Sera Kuhusu Kunakili Machapisho Haya

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi kinachohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* kinalindwa na Sheria za Haki Miliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali fulani, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kwenye mtandao kwa tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Dave Batty

Pendekezo Kuhusu Mpangilio Wa Kufundisha

Somo hili ni moja kati ya 14 katika mfululizo wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*. Masomo yote 14 yameorodheshwa hapa kama pendekezo la jinsi ya kuyafundisha. Mfuatano huu ulitayarishwa kwa ajili ya ufundishaji endelevu wa masomo haya. Tunaweza kuutazama kama picha ya gudurumu lenye vyuma kumi na vinne. Masomo haya hayategemei linalotangulia. Kila somo linasimama lenyewe. Basi, mwanafunzi anaweza kujiunga na madarasa wakati wowote na akaingia tu vizuri kwenye mfumo.

1. Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?
2. Kuitazama Biblia Kwa Haraka
3. Mtazamo
4. Majaribu
5. Maisha Ya Kikristo Yenye Mafanikio (ni pamoja na mafunzo juu ya huduma ya Roho Mtakatifu.)
6. Kukua kupitia kufeli
7. Matendo Ya Kikristo (Mahusiano Katika Kanisa La Mahali)
8. Utiifu kwa Mungu
9. Utiifu kwa Mwanadamu
10. Hasira na Haki za Kibinafsi
11. Jinsi Ya Kujifunza Biblia
12. Kujipenda na Kujikubali Mwenyewe
13. Mahusiano yako wewe Binafsi na Wengine
14. Nguvu Ya Kiroho na Mambo Yasio Ya Kawaida

Tazama kitabu kiitwacho, ***Kuwatanguliza waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***, ili kupata maelezo zaidi juu ya kufundisha masomo hayo.

Mipangilio ya Masomo

Kwa Mwalimu

Angalia ukurasa wa 4 wa Mwongozo wa Mwalimu kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya mipangilio hii ya masomo

Kulitazama Somo Kwa Ujumla

1. Ikiwezekana, gawa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* na *Mwongozo Wa Somo* siku moja au mbili kabla hujaanza kufundisha somo hili.

2. Katika ukurasa wa 11 wa huu mwongozo wa mwalimu utapata nakala ya ***Orodha Ya Kazi Za Darasani***, yenye kutoa tarehe ambapo kila kazi inapaswa kukamilishwa. Waambie wanafunzi wajaze tarehe husika wakitumia ile nakala tupu iliyoko katika *Mwongozo Wa Somo*.

3. Kwenye ukurasa wa 17 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* kuna orodha ya vitabu vya Agano Jipya, na migao yake. Wajulishe wanafunzi kutumia orodha hiyo wakati wanapojifunza kama maandalizi ya kufanya chemsha bongo za somo hili.

4. Unapofundisha somo hili, kazia ni kwa nini tunayo Biblia.

   A. Biblia haikuandikwa ili kuwa kitabu cha historia ya dunia nzima. Kweli, ina sehemu kubwa ya habari za kihistoria. Lakini, hilo silo kusudi kuu la Mungu kufanya Biblia iandikwe.

   B. Biblia haikuandikwa ili kuwa kitabu cha kutumiwa kutabiria wakati ujao.

   C. Ninahitaji kutumia mafundisho yaliyomo katika Biblia ili kunivuta mimi karibu na Mungu.

   D. Biblia inatakiwa kuwa kitabu cha kiada kwa ajili ya kuniongoza mimi katika mambo yangu ya kila siku.

   Rudia rudia sana kipengele C na D katika mafundisho yako yote. Vipengele hivi vinaweza kukusaidia ikiwa kutatokea ubishi kuhusu ni tafsiri gani ya Biblia iliyo bora kuliko zingine.

5. Epukana na jaribu la kufundisha kila kitu unachojua kuhusu mada hii. Kusudi letu hapa si kushughulikia kila kitu ambacho kinaweza kupatikana katika somo la Chuo cha Biblia – mfano, *Mapitio Ya Biblia 101*. Tunachotaka sisi ni kuweka msingi tu hapa na kuwalekeza kwingine wanakoweza kujifunza zaidi wao wenyewe.

6. Wazo moja linaloweza kuleta utofauti katika somo hili ni kuwatambulisha wanafunzi vitu mbalimbali vya kujifunza Biblia katika kila kipindi. Baadhi ya vitabu unavyoweza kuvifikiri ni kama kitabu cha ramani za Biblia, kitabu cha mafafanuzi, kitabu chenye orodha ya mada na mistari yake, Biblia zenye maelezo na mafunzo ya ziada, kamusi ya Biblia, na kitabu chenye habari zaidi kuhusu Biblia.

Orodha Ya Kazi Za Darasani

Mada ya Somo: Kuitazama Biblia Kwa Haraka

Chemsha Bongo

Utapewa chemsha bongo ya majina ya sehemu na vitabu vya Agano Jipya, kwa tarehe zinazo-orodheshwa hapo chini. Utapewa karatasi tupu na kutakiwa kuorodhesha sehemu na majina ya vitabu katika kila sehemu husika.

Tarehe	Siku Ya 1	Chemsha Bongo juu ya Injili na Historia ya Kanisa
Tarehe	Siku Ya 2	Chemsha Bongo Kuhusu Injili hadi Barua Za Paulo
Tarehe	Siku Ya 3	Chemsha Bongo juu ya vitabu vyote vya Agano Jipya na sehemu zake

Zoezi	Jina La Kazi	Tarehe ya Kuwasilisha
1	Vitabu Vya Musa	Siku Ya 1
2	Vitabu Vya Historia	Siku Ya 2
3	Vitabu Vya Ushairi	Siku Ya 2 Ukipenda
4	Manabii Wakuu	Ukipenda
5	Manabii Wadogo	Siku Ya 3
6	Injili Na Historia Ya Kanisa	Siku Ya 4
7	Barua Za Paulo	Ukipenda
8	Barua Za Jumla Na Kitabu Cha Unabii	Siku Ya 5

Mtihani Tarehe Siku Ya 5

1 Somo la 1
Sababu Ya Kuwa Na Biblia

1. Kweli Kuu ya KiBiblia

Nahitaji kuelewa kwa uwazi zaidi kwa nini tuna Biblia.

2. Mstari Mkuu: 1 Petro 2:2 Tafsiri Ya Lugha Rahisi

Kama watoto wachanga wanavyotaka maziwa, ninyi pia mnapaswa kutaka kunywa maziwa safi kabisa ambayo ni Neno la Mungu ili mkue na kuokolewa na adhabu ya dhambi.

3. Mahali Pa Mwanafunzi Kupata Haya

Sura ya 1 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* inaendana na somo hili.

4. Kuchangamkia Somo (Dakika 5-10)

Chagua shughuli mojawapo kati ya hizi 3 zifuatazo kutambulisha somo hili.

A. **Onyesha tafsiri mbalimbali za Biblia.** Ikiwezekana, uwe na nakala ya Agano la Kale kwa Kiebrania, na Agano Jipya kwa Kiyunani.

B. Uliza swali hili: **"Kama wewe ungekuwa Mungu,** na utake kuwa na kitabu kilichoandikwa kwa ajili ya binadamu hapa duniani, unadhani ni kitu gani kingekuwa cha maana zaidi kuwekwa katika kitabu hiki?" Darasa zima linaweza kujadili swali hilo kwa pamoja. Au, unaweza kuligawa darasa kwa vikundi vidogo vya watu wawili hadi wanne kwa ajili ya kujadili swali hili.

C. **Uliza Maswali Haya:**

Unakumbuka nini kutoka utotoni mwako kuhusu Biblia?
Je, nyumbani kwenu ilikuwepo Biblia?
Uliwahi kuisoma?
Wazazi wako na babu zako walikwambia nini juu ya Biblia?

Unaweza kuanzisha dara kwa kuwatia moyo wanafunzi wachache kushirikisha darasa majibu yao kwa maswali hayo. Au unaweza kuligawa darasa kwa vikundi vidogo vya watu watatu hadi watano ili kujadili maswali hayo.

5. Kweli Za Msingi Kuhusu Biblia (Dakika 5-10)

Shughulikia Hoja A, *"Kweli za msingi kuhusu Biblia."* Tazama ukurasa wa 5 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili upate habari hizo. Elezea zile hoja tatu za kwanza kwa ufupi.

6. Lugha Za Asili Za Biblia (Dakika 5-10)

Unapozungumzia ni lugha zipi zilizotumiwa kuandika Biblia hapo kwanza, unaweza kutaka kuwaonyesha wanafunzi nakala ya Agano la Kale kwa Kiebrania, na Agano Jipya kwa Kiyunani. Kama huna nakala hizo katika maktaba yako binafsi, basi tafuta kwenye makanisa yaliyoko jirani, vyuo vya Biblia, au maktaba za umma.

Hakikisha unaeleza sababu ya Agano la Kale kuandikwa kwa Kiebrania, na Agano Jipya kuandikwa kwa Kiyunani. Ni kwamba, hizo ndizo lugha zilizokuwa zinatumika na watu wa kawaida wakati vitabu hivyo vilipoandikwa. Vilevile, hiyo ndiyo sababu baadhi ya vitabu vya mwisho mwisho katika Agano la Kale viliandikwa kwa lugha ya Kiaramu.

7. Tafsiri Za Kiingereza Za Biblia Na Za Kiswahili (Dakika 5 hadi 10)

Huu unaweza kuwa wakati mzuri wa kutaja kwa ufupi jambo hilo hilo kuhusu tafsiri za Biblia. Siku hizi tunazo tafsiri nyingi za Biblia za Kiingereza na hata za Kiswahili. Sababu kubwa ya kuwa na tafsiri nyingi ni kwamba, watafsiri husika wanataka kutoa tafsiri sahihi ya Biblia katika lugha ya watu wa kawaida siku hizi.

Hapo mwanzo Biblia haikuandikwa kwa mtindo wa Kiingereza cha kale, au Kiswahili cha kale. Sababu ya Biblia hizo za kwanza kuonekana ngumu kueleweka na watu wengi ni kwamba, lugha hubadilika kadiri muda unavyokwenda. Tafsiri zilipofanywa miaka mia na zaidi iliyopita, mtindo huo wa lugha ndio ulikuwa kawaida na uliozoeleka na watu, na rahisi kwao kuelewa.

Pengine utatamani kuonyesha nakala ya Septuagint ambayo ni tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale, iliyokuwa inatumiwa sana huko Israeli siku za Bwana Yesu.

Angalia usikwame kwenye mjadala mkubwa wa kitaalam kuhusu tafsiri za Biblia. Nafasi yake iko baadaye. Kwa hapa, tunachotaka ni kutoa mtazamo mpana wa Biblia kwa ufupi.

Katika somo hili hatutaki kufikia mahali pa kuamua ni tafsiri ipi ya Biblia iliyo bora. Badala ya kufanya hivyo, tumia muda huu kusisitiza ni kwa nini leo tuna Biblia kwa lugha yetu.

Onyesha kwamba Mungu anajali sana sisi kutendea kazi kweli za Biblia katika maisha yetu ya kila siku, kuliko kujali tunasoma tafsiri gani ya Biblia. Njia nyingine ya kueleza hilo ni hii:

Tafsiri bora ya Biblia inayofaa kutumika ni ile *unayofanyia kazi* katika maisha yako ya kila siku.

1

8. Umoja wa Biblia Na Ufunuo Unaoendelea (Dakika 5-10)

Jadili Hoja B, *"Umoja wa Biblia,"* pamoja na Hoja C, *"Kuipata picha nzima (au, ufunuo unaoendelea)."* Tazama ukurasa wa 6 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili kupata habari za kueleza. Huna haja ya kuingia ndani sana kuhusu hizo.

Hoja C inashughulika na swala la kuwa makini kupata kweli yote wakati unaposoma Maandiko. Eleza kwa kifupi baadhi ya matatizo yatokanayo na "kuutoa mstari katika mazingira (mantiki) yake". Eleza tunamaanisha nini tunaposema hivyo.

9. Kristo anaingiaje katika Biblia nzima? (Dakika 5)

Tumia maelezo kwenye ukurasa wa 6 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili kufundisha juu ya Hoja D, *"Kristo anaingiaje katika Biblia nzima?"*

Hakikisha wanaelewa kwamba ufufuo wa Yesu Kristo ndilo tukio muhimu sana lililoandika katika Biblia. Sehemu hii ya somo inaweza kuunganishwa kirahisi sana na Kweli Kuu Ya KiBiblia ya somo hili.

10. Jinsi miaka inavyohesabiwa (Dakika 5)

Tumia maelezo kwenye ukurasa wa 7 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili kufundisha juu ya Hoja E, *"Jinsi miaka inavyohesabiwa."*

Baadhi ya wanafunzi wako wanaweza kuwa na ufahamu mdogo sana wa historia ya kale. Ni rahisi kueleza kwamba Agano la Kale liliandikwa kabla ya kuzaliwa kwa Yesu, na Agano Jipya liliandikwa baada ya kuzaliwa Kwake. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi wako huenda wasielewe jinsi tunavyohesabu miaka kabla ya kuzaliwa kwa Kristo.

Wanafunzi wako watakapoingia kwa mafunzo ya kina ya historia ya nyakati za Biblia, watahitaji kuwa na ufahamu ulio wazi na mzuri kabisa juu ya utaratibu huu wa kuhesabu miaka.

11. Kutendea somo kazi maishani (Dakika 5-10)

Pengine ni vizuri ufanye marudio ya *Kweli Kuu ya KiBiblia* pamoja na *Mstari Mkuu* unapohitimisha somo hili. Mwambie kila mwanafunzi atafakari juu ya maswali haya yafuatayo:

•Kwa nini Mungu alitupa Biblia?

•Ninataka niwe na Biblia kwa nini?

•Ninapanga kuitumiaje Biblia katika maisha yangu?

•Nitayaitikiaje (nitayapokeaje) mafundisho yaliyo katika Biblia?

Wanafunzi wanahitaji kuona kwamba Biblia ni barua ya Mungu kwetu. Yeye atazungumza nasi kupitia Neno Lake lililoandikwa.

12. Kazi za somo

A. Toa Chemsha Bongo ya Kwanza.

B. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 1, *"Vitabu vya Musa."*

C. Ikiwa hujafanya hivyo bado, gawa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* na *Mwongozo Wa Somo* wakati wa kipindi kuanza.

D. Waagize wanafunzi wasome Sura ya 1 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili kurudia mada zilizojadiliwa darasani siku ya leo.

E. Waagize wanafunzi wasome Sura ya 2 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* kama maandalizi kwa ajili ya kipindi kinachofuata.

13. Tathmini ya somo

Hebu andika mawazo yako kuhusu kuboresha hili somo.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

Somo la 2
Biblia Imevuviwa

2

1. Kweli Kuu ya KiBiblia

Kwa kuwa Biblia imevuviwa na Mungu, nahitaji leo kuitumia Biblia jinsi Mungu anavyoniambia.

2. Mstari Mkuu: 2 Timotheo 3:16

Maandiko yote yamevuviwa na Mungu, na yanafaa kwa ajili ya kufundisha imani na kurekebisha makosa, kwa ajili ya kutoa mwelekeo mpya wa maisha ya mtu, na kumfundisha kwa ajili ya kuishi vizuri.

3. Mahali Pa Mwanafunzi Kupata Haya

Sura ya 2 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* inaendana na somo hili.

4. Kuchangamkia Somo (Dakika 5)

Chagua shughuli moja au zote zifuatazo ili kutambulisha somo. Ukiamua kutumia igizo, utahitaji kuwachagua washiriki mapema na kuwaelekeza sehemu wanazotakiwa kuigiza.

A. Herufi Katika Mfuko

Utahitaji kupata mchezo uitwao *Scrabble* au wewe uandae mchezo huu: Andika herufi zote 26 za alfabeti – kila moja peke yake kwenye vikadi au karatasi ngumu kidogo. Tia herufi zote ndani ya mfuko, kisha tingisha mfuko wenyewe. Halafu, mwaga herufi zote juu ya meza. Zisambaze ili zisilaliane. Jaribu kuangalia ni maneno mangapi au sentensi ngapi zimetokana na hizo herufi bila kuzipanga. Hutapata neno wala sentensi hata moja.

Tumia onyesho hilo dogo tu kusisitiza hoja kwamba, Biblia haikutokea na kuwa kama ilivyo kwa bahati tu. Mmoja – ambaye ni Mungu – aliipanga na kuitayarisha iwe kama ilivyo kwa kuwatumia watu wengi mbalimbali kukamilisha kazi hii.

B. Igizo Fupi Kwa Ajili Ya "Waandishi Wa Habari"

Waambie wanafunzi kwamba wataona watu wawili wakikutana. Wao sehemu yao ni kuwa waandishi wa habari wa kuandika kilichotokea mara tu baada ya igizo kumalizika. Wasilinganishe taarifa walizoandika mpaka kila mtu amalize.

Kwa ajili ya igizo, watayarishe watu wawili waingie darasani kutoka pande tofauti, na wakutane mbele ya wenzao. Mmoja awe mcheshi na mwenye furaha, na aseme, "Vipi wenzangu? Hamjambo? Habari za leo?" au vyovyote atakavyoona afanye. Yule wa pili aingie akiwa amenuna . Asimjibu vizuri yule mtu wa kwanza. Halafu, wote waondoke.

Waambie wanafunzi kwa mara nyingine tena waandike walichoona kikitokea. Usiruhusu mjadala wa aina yoyote au kuzungumza. Wakimaliza taarifa yao, toa nafasi kwa kila mmoja kusoma taarifa yake. Bila shaka taarifa zitafanana, lakini hakuna zitakazofanana moja kwa moja, neno kwa neno, toka mwanzo hadi mwisho.

Tumia taarifa zao kuonyesha ukweli kwamba Mungu alitumia watu wengi mbalimbali kuandika vile vitabu 66 katika Biblia. Leo tutatazama jinsi Mungu alivyofanikisha jambo hili.

5. Uvuvio – Ni nini Maana Yake? (Dakika 5 - 10)

Lengo lako la kwanza leo ni kuwasaidia wafikie uelewa mzuri wa maana ya "uvuvio". Mwambie mwanafunzi mmoja atazame kamusi, na asome tafsiri inayotolewa ya neno hili.

Vuvia *(*Kwa mujibu wa Kamusi iitwayo *Webster's Intermediate Dictionary)*

(1) kuhimiza, kuongoza au kufanya mawasiliano kwa ushawishi wa kiMungu au usio wa kawaida <manabii walivuviwa na Mungu> <mawazo yamevuviwa na Mungu>

(2a) kuwa na ushawishi kwa mtu au kitu, wenye kusisimua, kuhuisha au kukuza <amevuviwa na mama yake>

(2b) kuathiri <utotoni alivuviwa akawa na shauku ya kupata elimu>

(2c) kuingiza au kufanya iingie mawazoni: kuamsha <huvuvia imani ndani ya wafuasi wake>.

Toa mifano kadhaa kuonyesha jinsi tunavyotumia neno hili katika mazungumzo yetu ya kawaida kila siku.

- uzuri wa jua kuchwa humvuvia mchoraji kuchora picha ya tukio hilo.
- Kiongozi wa kisiasa huwavuvia makutano kwa hotuba yake yenye nguvu.
- Kusoma kitabu humvuvia kijana kufuata njia aliyopitia shujaa wake (au, mtu anayeiga mfano wake).

Sasa, tunaposema Mungu aliwavuvia watu kuandika vitabu vya Biblia, tunamaanisha nini? Hapo tunazungumzia juu ya kitu maalum – kilicho tofauti kabisa na swala la jua kuchwa, au kiongozi wa siasa, au swala la kusoma kitabu.

6. Kuvuviwa Kwa Biblia (Dakika 5 - 10)

Wanafunzi watafute na kusoma 2 Timotheo 3:16 na 2 Petro 1:20-21. Ikiwezekana, mistari hiyo isomwe kutoka tafsiri kadhaa tofauti. Hebu tazama ukurasa wa 8-9 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili kupata habari zaidi juu ya hoja hii.

Kwa muhtasari, eleza uliyogundua kwa kuwapa maana ya uvuvio wa KiBiblia itolewayo katika ukurasa wa 9 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi*.

Tunaposema "Biblia imevuviwa na Mungu" tunamaanisha kwamba:

Roho Mtakatifu aliongoza mawazo ya waandishi kuandika yale Mungu aliyotaka waandike.

2

7. Bango Kuhusu Uvuvio

Andika tafsiri ya uvuvio KiBiblia itokayo kwa ukurasa wa 9 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* kwenye karatasi kubwa, kisha uitundike darasani mwako mahali ambapo ni rahisi kwako kurejea tena na tena katika kipindi hiki cha darasa.

Sisitiza lile jambo linalotajwa katika ukurasa wa 9 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi*.

"Ni muhimu sana kuelewa kwamba Biblia yote nzima imevuviwa na Mungu. Vitabu vyote vimevuviwa na Mungu kwa kiwango sawa. Hakuna vitabu vingine "vilivyovuviwa zaidi" ya vingine."

8. Jadili Hoja B. Mungu aliwavuviaje watu waandike vitabu vya Biblia? (Dakika 10-20) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 9-10

Shughulikia zile hoja tatu za ukurasa wa 9 na 10 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* zinazoeleza jinsi Roho Mtakatifu alivyowavuvia watu husika waandike vitabu vya Biblia. Wakati wa kuzungumzia hoja ya tatu kwamba *"Roho mtakatifu aliwapa mawazo ambayo wao waliyafafanua kwa namna yao wenyewe,"* rejea ile shughuli ya kufungua kipindi – lile igizo la "waandishi wa habari."

Onyesha kwamba kila mmoja wa walioandika Biblia alikuwa na mtindo wake wa uandishi. Lakini Mungu aliwaongoza mawazo yao kwa uzuri kabisa, na kwa sababu hiyo hawakuingiza habari ambazo si sahihi, ambazo Mungu hakutaka ziwemo kwa Biblia.

9. Jadili Hoja C-1. Vitabu vya kwanza viliandikwaje? (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 10

Ukurasa wa 10 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* hutoa habari za msingi ili kufafanua hili. Elezea vizuri tu kwamba zile nakala za mwanzo kabisa za vitabu vya Biblia hazipo. Tulizo nazo ni nakala za zamani sana za vitabu hivyo.

10. Jadili Hoja C-2. Je, vitabu vya Biblia vilinakiliwaje? (Dakika 5 hadi 10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 10

Toa ile habari ya ukurasa wa 10 kwenye *Mwongozo Wa Mwanafunzi* chini ya hoja ndogo namba 2, *"Je, vitabu vya Biblia vilinakiliwaje?"* Ikiwezekana, njoo darasani na picha za magombo yaliyotumiwa. Kuna vitabu vingi sana siku hizi kuhusu yale magombo maarufu ya Dead Sea. Pia, vitabu vingi vya fafanuzi za Biblia vitakuwa na habari juu ya magombo hayo.

Pengine utataka kuwapa habari zaidi juu ya masharti ambayo waandishi walionakili walitakiwa kuzingatia wakati wa kunakili vitabu vya Biblia. Tafadhali ona kwamba katika somo linalofuata (Sura Ya 3), *"Nawezaje kujua kwamba Biblia ni sahihi?"* kuna kijisehemu kinachozungumzia yale Magombo ya Dead Sea. Ukiona kama muda wa darasa unakwishia, pengine usubiri mpaka utakapofundisha somo husika ili ushughulike na mada hiyo.

Onyesha kwamba siku hizi watafsiri wa Biblia wana mamia ya nakala za zamani za Kiebrania na Kiyunani kwa ajili ya kuzitumia wakati wa kufanya tafsiri mpya za Biblia.

11. Kutendea somo kazi maishani (Dakika 5-10)

Katika sehemu hii leo, rudia tena Kweli Kuu ya KiBiblia na ule Mstari Mkuu wa somo hili. Watie wanafunzi moyo kujitolea kuiamini Biblia na kuikubali kuwa ni Neno la Mungu. Si mawazo mazuri tu ya wale Wayahudi walioiandika.

Watie moyo kutafuta njia ambazo ni halisi za kuanza kutumia mafundisho ya Biblia katika maisha yao kila siku.

12. Kazi za somo

A. Toa ile Chemsha Bongo ya Pili inayohusu Injili hadi Barua Za Paulo.

B. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 2, *"Vitabu vya Historia,"* na Mwongozo Wa Somo Zoezi la 3, *"Vitabu vya Ushairi."*

C. Wanafunzi wasome Sura ya 2 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili kurudia mada zilizojadiliwa darasani leo.

D. Wanafunzi wasome Sura ya 3 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* kama maandalizi kwa ajili ya kipindi cha somo kinachofuata.

13. Tathmini ya somo

Hebu andika mawazo yako kuhusu kuboresha hili somo.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

Somo La 3
Je, Biblia Ni Sahihi?

3

1. Kweli Kuu ya KiBiblia

Nahitaji kuthibitisha katika maisha yangu ya kila siku kwamba, mafundisho ya Biblia ni kweli.

2. Mstari Mkuu: Marko 4:24 Tafsiri Ya Lugha Rahisi

Hakikisheni kwamba mnafanyia kazi yale mnayosikia. Kadiri mtakavyofanya hivyo, ndivyo mtakavyoelewa zaidi ninayowaambia.

3. Mahali Pa Mwanafunzi Kupata Haya

Sura ya 3 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* inaendana na somo hili.

4. Kuchangamkia Somo: Igizo la mtu mwenye kiu (Dakika 5)

Kabla ya darasa kuanza, chagua watu wawili washiriki katika igizo hili. Leta darasani chupa mbili zinazofanana. Zote zijaze maji.

Mwambie yule mtu wa kwanza aziweke hizo chupa mbili zenye maji juu ya meza, na ueleze anachofanya na yale maji yaliyomo ndani mwa chupa. Chupa moja itakuwa na maji safi, na ile nyingine tutasema ina sumu. Kwa chupa moja ongezea matone machache ya kitu tutakachosema ni sumu. Hata spiriti inafaa.

Mhusika asome kwa sauti ile sehemu kwenye chupa inayosema mtu asiinywe. Aweke namba kwenye kila chupa ili ajue ni ipi yenye sumu. Halafu, aketi karibu na maji hayo na aanze kusoma gazeti.

Yule mtu wa pili aingie kutoka nje ya darasa na kusema, “Ninasikia kiu. Je, una chochote ninachoweza kunywa?”

Yule mwenye maji aseme, “Ndiyo. Nina chupa mbili za maji hapa. Moja ina maji safi, na nyingine ina sumu ndani yake. Kama unataka maji, jihudumie.” Kisha achukue gazeti lake aendelee kusoma.

Sasa, yule mwenye kiu anasita, kisha anachukua zile chupa mbili na kuzitazama kwa makini sana. Halafu aseme, “Unanitania, sivyo? Hakuna sumu yoyote katika maji haya!”

Mtu mwenye gazeti anasema, “Hapana, sikutanii hata kidogo. Moja ya hizo chupa ina sumu. Ninajua kwa sababu mimi ndiye nimeiweka. Ila, ile nyingine ina maji safi kabisa – tena ni matamu kweli! Bila shaka nimekusikia vizuri ukisema una kiu, sivyo? Wewe jihudumie.”

Yule mwenye kiu anasema, “Nitajuaje unaniambia ukweli? Labda umetia sumu kwenye chupa zote mbili? Nitajuaje kwamba nikikuuliza ipi ni salama kunywa utaniambia ukweli? Pengine wewe ni mtu mgonjwa sana, unayependa kuona watu wakifa.”

Yule mtu wa kwanza anaweka gazeti lake chini na kusema, “Mimi si mgonjwa. Ni mtu anayeaminika. Ninafanya hivi ili kuwafundisha hawa wanafunzi somo muhimu sana. Mimi sidanganyi. Sipendi kukuona ukinywa sumu. Ndiyo sababu nimekwambia chupa moja ina sumu. Kama unataka maji, itabidi uniamini.” Anapochukua ile chupa yenye maji safi, anamwambia, “Haya! Chukua unywe. Hii ni salama kunywa.” Kisha wote wawili waondoke pale mbele.

5. Kuingia kwa somo kutoka kwa igizo (Dakika 2-5)

Wote tunahitaji maji ya kunywa, kama tunataka kuendelea kuwa hai kimwili. Lakini, tukitaka kupata uzima wa kiroho utakaodumu milele, lazima tukubali kumwamini Mungu anaposema, “Niaminini Mimi. Ninao uzima wa kuwapa. Neno langu lililoandikwa – yaani Biblia – limejaa ukweli. Mnaweza kuliamini. Wekeni matumaini yenu kwa hilo Neno.”

Lakini, wengi wetu huuliza, “Nawezaje kujua kama Biblia ni sahihi? Nitajuaje kwamba Biblia haijabadilishwa? Labda imejaa makosa. Je, mnaweza kuthibitisha kwamba Biblia haijachakachuliwa na watu ikabadilishwa?”

Kusudi kuu la somo hioli ni kutafuta ushahidi wenye uhakika unaoonyesha kwamba Biblia tuliyo nayo leo ni sahihi na ni kweli.

6. Jadili Hoja A, Unabii wote ndani yake umekuwa wa kweli na sahihi kabisa: Unabii Wa Agano La Kale
(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 11

Kwanza, eleza unabii ni nini. *Mwongozo Wa Mwanafunzi* unatoa tafsiri zifuatazo ukurasa wa 11:

(1) Ni ujumbe kutoka kwa Mungu, unaotolewa na Mkristo.

(2) Ni utabiri – Ujumbe toka kwa Mungu, unaoeleza kitakachotokea wakati ujao.

Tazama ukurasa wa 11 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* kwa maelezo zaidi juu ya jambo hili. Waambie wanafunzi watafute na kusoma unabii kadhaa kutoka Agano la Kale, na mahali katika Agano Jipya penye kueleza kutimizwa kwake. Onyesha kwamba baadhi ya yale magombo ya Dead Sea yamethibitishwa kuwa yaliandikwa kiasi cha miaka hata 200 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu. Hivyo, tunajua kwamba unabii huu uliandikwa kabla ya kutimizwa kwake.

7. Jadili Hoja A, Unabii wote ndani yake umekuwa wa kweli na sahihi kabisa: Unabii Wa Agano Jipya
(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 11

Injili pia zina unabii uliotimizwa kwa kufa na kufufuka kwa Yesu. Waweza kuwa na maandishi ya ziada yenye kuonyesha jinsi ambavyo isingewezekana kwa unabii wote uliotimizwa katika Biblia kutimizwa kwa mbinu zozote, au kibinadamu. Onyesha kwamba hakuna unabii hata mmoja ambao umeonekana kuwa wa uongo.

Ushahidi unaopatikana unaelekea kuunga mkono Biblia inayoaminika. Neno la Mungu linaweza kuaminiwa. Linaposema kuna uhai baada ya kifo, na kwamba tunachagua mahali pa kukaa milele wakati huu, tunahitaji kufikiri kwa makini sana jinsi tutakavyoitikia habari hizo.

8. Jadili Hoja B. Biblia inasema ni Neno la Mungu
(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 11

Tazama ukurasa wa 11 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili upate maandiko na maelezo kuhusu mada hii. Wanafunzi wanahitaji kutambua kwamba kama tutaweza kuthibitisha kwamba Biblia si Neno la Mungu, basi tunaweza kuyapuuza mafundisho yake. Lakini yenyewe inadai kwa uwazi kabisa kuwa ni kitabu cha Mungu, si kitabu cha wanadamu.

9. Jadili Hoja C. Yesu alisema Biblia ni Neno la Mungu
(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 12

3

Tazama ukurasa wa 12 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili upate habari na maandiko ya kutumia kufafanua mada hii. Hapa angalia usinaswe kwenye mjadala wenye hoja zinazoonekana kuwa halali, za muda mrefu. Pamoja na hayo, unaweza kujenga hoja yenye nguvu juu ya ushuhuda wa Yesu. Kama inawezekana Yeye kuthibitishwa kwamba ni mwenye dhambi au ni mwongo, basi tunaweza kutupilia mbali kila kitu. Lakini kama alichosema ni kweli, basi tunahitaji kuangalia sana hali yetu ya mioyo kuhusu Maandiko.

10. Jadili Hoja D. Katika Biblia hakuna kupingana
(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 12

Eleza kupingana ni kitu gani ili uwe na uhakika kwamba wanaelewa unachozungumzia hapa. Tazama ukurasa wa 12 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili kupata habari juu ya mada hii.

Unaweza kupenda kutumia kielelezo hiki ili kuonyesha jinsi watu wanavyofanya kosa la kuona kwamba Biblia ina maeneo ambapo inapingana.

Waulize wanafunzi swali hili: “Fikirieni kitakachotokea kwa imani yenu kuhusu Mungu ikiwa nitaweza kuthibitisha kwamba Biblia inasema, ‘Hakuna Mungu.’ Mnakataa? Hebu mmoja atafute na kusoma Zaburi ya 14:1”. Waambie watazame mstari huo na kujionea wenyewe kinachosemwa hapo.

Zungumza nao matatizo yanayotokea wakati watu wanapochukua sehemu tu ya mstari, badala ya kuangalia mantiki kamili. “Kupingana” kwingi kunakosemwa na watu kunaweza kuelezwa kwa kutazama kwa makini sana kinachosemwa na Biblia juu ya swala husika.

Watahadharishe wanafunzi wako juu ya tatizo lingine la kawaida hapa. Wengi wanaoamini kwamba Biblia inapingana watasema, “Biblia inajipinga yenyewe.” Wataendelea na kukuambia “kupingana” kwenyewe. Waambie wanafunzi wamwulize mtu kama huyo ataje mahali palipo na “kupingana” huko – yaani kitabu, sura, na mstari katika Biblia. Wengi hawana yote hayo. Waambie watazame vizuri Biblia inasemaje hasa.

11. Jadili Hoja E. Akiolojia inathibitisha kwamba Biblia ni sahihi (Dakika 10-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 13

Mada hii imeshughulikiwa vizuri katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ukurasa wa 13. Unaweza kuleta vitabu kadhaa darasani vinavyoshughulikia na nada hii. Ushahidi katika taaluma hii ni mwingi, tena wenye nguvu sana. Magombo ya Dead Sea ndiyo uvumbuzi muhimu sana katika karne ya ishirini. Pengine umekwisha zungumzia Magombo ya Dead Sea katika mojawapo wa somo lililotangulia.

Leta picha za hayo magombo ili wanafunzi wako wayatazame. Vitabu vya mafafanuzi ya Biblia vya hivi karibuni vinavyohusu Biblia vitakuwa na picha zake. Kama huna vitabu aina hii, wasiliana na mchungaji wako au nenda kwenye maktaba ya umma iliyo karibu nawe.

3

12. Jadili Hoja F. Taratibu za kimatibabu katika Biblia zinaithibitisha kwamba ni sahihi (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 13

Tazama ukurasa wa 13 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili upate habari zaidi juu ya mada hii. Kitabu kile kiitwacho *None of these Diseases*, kilichoandikwa na S.I. McMillen ambaye ni tabibu (au daktari), hutoa ushahidi wa kusisimua sana katika eneo hili. Hebu shirikisha mifano miwili au mitatu kutoka kitabu hiki kuonyesha jinsi miaka elfu nyingi iliyopita, Mungu alitoa sheria za kitabibu katika Biblia, ambazo ziko sahihi kabisa kimatibabu.

Onyesha jinsi tamaduni nyingi za wakati huo zilizokuwa zimeendelea sana zilivyokuwa na sheria za kimatibabu ambazo hazikuwa salama, na mara nyingi zilisababisha kifo, si uponyaji. Kama ungependa kununua nakala ya kitabu hiki, waandikie wahusika walio kwa Ofisi ya Mitaala ya Teen Challenge USA.

13. Jadili Hoja G. Wewe mwenyewe jithibitishie kwamba Biblia ni ya kweli kwa kupima mafundisho yake katika maisha yako (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 14

Pengine hiki ndicho kipimo chenye nguvu zaidi kinachoweza kutumika kuthibitisha usahihi wa Biblia. Vile vingine vyote ni vya kiakili kwa kiasi Fulani. Lakini hiki ni cha kibinafsi kabisa.

Toa mifano michache ya binafsi, kutoka maishani mwako au kwa Wakristo wengine unaowajua. Onyesha jinsi fundisho fulani katika Biblia limekuwa kweli maishani mwako. Usitumie kweli ya jumla tu ya Biblia. Lenga kitu halisi.

Watie moyo wengine darasani kushirikisha mifano binafsi jinsi ambavyo wamethibitisha mafundisho ya Biblia katika maisha yao.

Pia, waweza kumhoji Mkristo wa siku nyingi (au mhitimu mmojawapo wa Teen Challenge, kama unafundisha somo hili katika kituo cha Teen Challenge), na utoe nafasi kwao kukupa mifano binafsi jinsi ambavyo wao wamethibitisha kuwa Biblia ni kweli.

Tazama ukurasa wa 14 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili kupata habari zaidi na Maandiko juu ya mada hii. Jambo moja tunalotaka kusisitiza ni kwamba Biblia si kitabu cha manuizo na uchawi. Si kwamba utasema tu mstari mmoja wa Biblia na uone muujiza fulani ukitokea.

Biblia imejaa ushauri halisi kwa ajili ya maisha ya kila siku. Luka 6 na Warumi 12 kuna mafundisho tele halisi yanayoweza kupimwa katika maisha. Lakini sababu kubwa ya Mungu kuweka mafundisho hayo hapo ni kuwasaidia watu – si kufanya yawe majaribio kwa ajili ya watu wabishi na wasiotaka kuelewa ukweli.

3

Ni kitu kisicho na faida yoyote kumdai Mungu ajithibitishe kama kweli yupo kwa kufanya kile tunachomwambia afanye. Yeye ni Bwana – ni Mtawala. Kama kuna mtu wa kutoa madai, anapaswa kuwa Mungu, sio sisi. Onyesha kwamba utii ndiyo siri ya mafanikio katika eneo hili. Makusudi yetu ya moyoni pia ni muhimu sana.

14. Jedwali (au Mchoro) ya Mfumo Wa Kujifunza Biblia Wa Maisha Kwa Maisha (Dakika 5-10)

Utaikuta ile Jedwali ya *Mfumo Wa Kujifunza Biblia Wa Maisha Kwa Maisha* kwenye ukurasa wa 25 wa mwongozo huu wa mwalimu. Mfumo huu unaweza kutumiwa kuhusisha Maandiko kwa matatizo ambayo mtu anayakabili maishani mwake. Pengine utapenda kupitia eneo hili pamoja na wanafunzi wako, ukitumia mifano kadhaa kutoka maishani mwako.

15. Kutendea somo kazi maishani (Dakika 5-10)

A. Pengine ni vizuri kuunganisha sehemu hii ya somo na shughuli namba 13 na 14 katika mpango wa kufundishia somo hili. Watie moyo wanafunzi wako kujihusisha na kushughulika kikamilifu kabisa katika *Mfumo Wa Kujifunza Biblia Wa Maisha Kwa Maisha* kwa maeneo maalum katika maisha yao wenyewe. Waambie waandike matokeo walipofanyia kazi mistari hii katika maisha yao.

B. Swali jingine unaloweza kuwapa ili wafikiri zaidi ni hili: Je, usahihi wa Biblia unapaswa kugusa maisha yangu kwa njia gani leo? Yafuatayo ni mawazo matatu yanayoweza kuwa itikio la swali hilo:

1. Ninaweza kuitegemea Biblia na kuiamini kwamba kweli ni Neno la Mungu.

2. Ninaweza kuamini kwamba kinachosemwa na Biblia leo ni kile kile Mungu alichowaambia wale walioandika Biblia hapo mwanzoni.

3. Ninahitaji kuwa makini katika kutumia kwa usahihi mafundisho ya Biblia katika maisha yangu leo.

Mfumo Wa Kujifunza Biblia Wa Maisha Kwa Maisha

1. Niorodheshe **hali zinazoleta wasiwasi**
   —hali zinazofanya iwe rahisi kwangu kuvimba, kupoteza mwelekeo, kukasirika, kuudhika, kuvunjika moyo, au ninapojisikia kubanwa na kusongwa.

2. **Nimuulize Mungu** swali hili:
   —"Ee Mungu, ni nini unachojaribu kunifundisha **nifanye leo**?"

3. Nitafute eneo moja katika maisha yangu ya kila siku ambapo **ninataka kukua**
   —tumia 1 Wakorintho 13:4-8 kugundua au kutambua maeneo ninayohitaji kukua.

4. Nihusishe hili katika **kujifunza Biblia** kwangu
   —je, Biblia ina lipi la kusema juu ya eneo hili maishani mwangu, ninalohitaji kukua?

5. **Niorodheshe vitu** ninavyoweza kumaliza leo
   —yaani, weka malengo
   —chagua lengo moja na ulitende leo

6. **Tathmini** matokeo

   —baadaye siku hiyo hiyo au siku inayofuata, rejelea mambo uliyofanya uone ni nini kilichotokea ulipojaribu kufikia lengo ulilojiwekea.

3

Jedwali hii hii au iliyorekebishwa kidogo inatumika katika masomo yafuatayo katika Mfululizo huu wa *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya.*

1. Matendo Ya Kikristo, somo la pili
2. Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo, somo la nane na tisa
3. Jinsi Ya Kujifunza Biblia, somo la pili
4. Maisha Ya Kikristo Yenye Mafanikio, somo la pili

16. Kazi Za Somo

A. Toa Chemsha Bongo ya vitabu vyote vya Agano Jipya, na majina ya migao yake.

B. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 5, *"Manabii Wadogo."*

C. Waambie wanafunzi wasome Sura ya 3 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* kama marudio ya mada zilizofundishwa darasani leo.

D. Wanafunzi wasome Sura ya 4 na ya 5 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* kama maandalizi kwa ajili ya kipindi kifuatacho cha darasa.

17. Tathmini ya somo

Hebu andika mawazo yako kuhusu jinsi ya kuboresha somo hili.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

Somo La 4
Kutazama Agano La Kale Na Jipya Kwa Kifupi

4

1. Kweli Kuu ya KiBiblia

Nahitaji kuitumia Biblia inisaidie katika mambo yote ninayopitia kila siku.

2. Mstari Mkuu: 2 Timotheo 3:17

Maandiko ndiyo vifaa kamili vya mtu a Mungu, nayo humtosheleza kikamilifu kabisa kwa ajili ya kila eneo la kazi yake.

3. Mahali Pa Mwanafunzi Kupata Haya

Sura ya 4 na ya 5 katika *Mwongozo Wa Mwanafunzi* zinaendana na somo hili. Kazi zozote za Mwanafunzi zilizomo katika *Mwongozo Wa Somo* zinaweza kutumiwa kwa somo hili.

4. Kusudi la somo hili

Katika somo hili, lengo letu kuu ni kutoa muhtasari mdogo tu wa Agano la Kale na Agano Jipya. Baadhi ya wanafunzi wetu huenda wasiwe na picha nzuri sana ya jumla kuhusu Biblia. Wakiweza kuipata “picha kubwa” kwa leo, basi itakuwa rahisi kwao kuelewa jinsi vitabu hivyo tofauti vyote vinavyoingia katika mpango wa Mungu kwa ajili ya dunia yetu. Mwisho wa somo hili utapata nafasi ya kuzungumzia kazi na nafasi ya unabii kwa wakati wetu ujao.

5. Mtiririko wa historia ya dunia

Pengine utahitaji kutumia maelezo juu ya mtiririko wa historia ya dunia ili kuonyesha Biblia inatuambia nini kuhusu historia ya dunia. Mtiririko huo uhusishe haya yafuatayo:

•uumbaji

•matukio ya kwanza kwanza katika kitabu cha Mwanzo

•Nuhu na gharika

•mnara wa Babeli

•kuitwa kwa Ibrahimu

•Yusufu akiwa Misri

•Musa akiwaongoza Wayahudi kutoka Misri

•Israeli chini ya waamuzi

•utawala wa:

Mfalme Sauli

Mfalme Daudi

Mfalme Sulemani

•kugawanyika kwa Israeli kuwa mataifa mawili

•kipindi cha uhamisho huko Babeli

•kurejeshwa kwa mataifa ya Israeli

•miaka 400 ya ukimya kati ya Agano la Kale na Agano Jipya

•maisha ya Yesu

•kuanzishwa na kusimama kwa kanisa huko Yerusalemu

•safari za Paulo za kimishenari

•matukio duniani kwa wakati ujao, kama yalivyoandikwa katika kitabu cha Ufunuo.

Tumia huo mtiririko wa wakati kwa muda wote wa somo, ukionyesha ni vitabu gani vya Biblia vinaingiana na kila kipindi. Si lazima sana upate tarehe sahihi za kila kitabu kwenye maelezo yako ya mtiririko, lakini jaribu kuonyesha muda wa kiujumla tu ambapo kila mgao wa vitabu uliandaliwa. Eleza kwa kifupi kusudi la aina mbalimbali za vitabu vilivyomo katika Biblia.

6. Kulitazama Agano La Kale Kwa Kifupi (Dakika 10-20)

Katika ukurasa wa 15 na 16 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* utapata habari za msingi kuhusu Agano la Kale, zinazoweza kutumiwa hapa. Eleza kwa kifupi kwa nini neno “agano” linatumika kueleza hizo sehemu kuu mbili za Biblia. Katika 1 Wakorintho 10:11 kuna maelezo mazuri sana kwa nini Agano la Kale ni muhimu kwetu sisi leo.

Vilevile unaweza kutaka kurejelea baadhi ya maswali kutoka kwa Kazi walizokamilisha katika *Mwongozo Wa Somo* kwa ajili ya mafunzo haya.

Onyesha kwamba katika siku za Yesu hapa duniani, Biblia pekee waliyokuwa nayo watu wale ni Agano la Kale. Sisi tunahitaji kuwa makini tusipunguze thamani ya Agano la Kale. Watie moyo wanafunzi kulisoma Agano la Kale kwa njia ambayo hawatachoshwa nalo. Siri ya kufanikiwa kwa hilo ni kusoma vitabu tofauti tofauti, badala ya kufululiza.

Watie moyo kusoma Agano la Kale pamoja na Agano Jipya, na kuhama kutoka aina moja ya uandishi hadi nyingine. Watie moyo wanafunzi wako kusoma vitabu na kuvimaliza kwa wakati mmoja badala ya kuhama hama kwenda sura tofauti na kitabu kingine kila siku.

7. Kuitafsiri Biblia

Baadhi ya vitabu vya Biblia vinaweza kumchanganya mtu, katika kutafuta jinsi ya kuvitafsiri. Gordon Fee na Douglas Stewart wameandika kitabu kiitwacho *How to Read for All its Worth: A Guide to Understanding the Bible,* ambacho hutoa mtazamo mzuri sana kuhusu swala hili. Kitabu chenyewe kimeandikwa kwa ajili ya watu wa kawaida (yaani, ambao si wasomi wa Biblia), lakini kinaweza kuwa kigumu kwa baadhi ya wanafunzi wako.

8. Kulitazama Agano Jipya Kwa Kifupi (Dakika 10-20)

Shughulika na Agano Jipya kwa namna ileile uliyotumia kushughulikia Agano la Kale. Pia, fikiria kutumia baadhi ya maswali yatokayo kwa Kazi zao za Kufanya katika *Mwongozo Wa Somo*.

4

9. Nafasi na kazi ya unabii katika Biblia (Dakika 5-15)

Eleza kwa ufupi ni kwa nini Mungu aliweka unabii katika Biblia. Hii ni hoja ya muhimu sana kuitoa katika sehemu hii ya somo. Mara nyingi majadiliano kuhusu unabii huwa ni juhudi za kujaribu kujua mambo yote yanayohusiana na matukio ya wakati ujao. Eleza vizuri tangu mwanzo kwamba Mungu hakuweka unabii katika Biblia ili tupite-pite tukibashiri wakati ujao kama wanavyojaribu kufanya wanajimu wa siku hizi.

Mungu aliweka unabii katika Biblia kwa sababu zifuatazo.

1. Kuonyesha usahihi wa Biblia.
2. Kuwapa Wakristo tumaini katika wakati ujao. Warumi 15:4
3. Kuwahamasisha watu kumkaribia Mungu zaidi.
4. Usitumiwe kutabiri kuhusu wakati ujao.

Ona itikio la Yesu kwa Petro, wakati alipojaribu kumfanya Yesu ampe maelezo kuhusu wakati ujao. Tazama Yohana 21:15-24, hasa mstari wa 20 hadi 23. Pia, ona jinsi ambavyo watu walitafsiri vibaya kwa urahisi kabisa maneno ya Yesu juu ya wakati ujao wa Yohana. Sisi pia tunaweza kufanya kosa hilohilo tukianza kutumia unabii vibaya.

10. Kutendea somo kazi maishani (Dakika 5-10)

Tumia ile Kweli Kuu Ya KiBiblia ya somo la leo kusisitiza haja ya kila mmoja wetu kutumia kwa makini sana Neno la Mungu kama kiongozi katika maisha yetu ya kila siku. Limejaa mambo yanayotia moyo, mwelekeo, na maonyo. Kama tutaliheshimu na kulitii, tutagundua kwamba mahusiano yetu na Mungu yatakuwa ya kina, pamoja na kukua.

Kwa upande mwingine, tunapaswa kukumbuka kwamba upendo wetu na heshima yetu kuu si kwa kitabu, bali kwa mwandishi wake – yaani Mungu Mwenyewe.

11. Kazi za somo

Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 6, *"Injili Na Historia Ya Kanisa,"* na kazi zingine zozote wanazoweza kuwa wamemaliza, ambazo hujasahihisha.

12. Tathmini ya somo

Hebu andika mawazo yako kuhusu kuboresha somo hili.
Ni sehemu zipi zilizokuwa nzuri?
Ni sehemu zipi ambazo wanafunzi wamepata shida kuzielewa?
Ni sehemu zipi zilizokuwa za msaada sana kwa wanafunzi wako?

Somo La 5
Mtihani

1. Utangulizi

Fanya utangulizi wa somo litakalofuata.

A. Wape Mwongozo wa Somo au Mazoezi yoyote ambayo yanapaswa kukamilishwa kabla ya kipindi cha kwanza cha kozi ifuatayo utakayofundisha.

B. Waelekeze wanafunzi kufungua ukurasa wa mwisho katika Mwongozo wa Somo Mpya. Wanapaswa kupata nakala safi ya ***Orodha ya Kazi za Darasani.***
Wape tarehe za majaribio ya chemsha bongo, Zoezi, na mtihani.

C. Wape Mwongozo wa Mwanafunzi mpya na uwaambie kurasa watakazosoma kabla ya kipindi kifuatacho darasani.

2. Wape mtihani wa Somo hili.

3. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 8, *"Barua Za Jumla Na Kitabu Cha Unabii."*

4. Ikiwa hujafanya hivyo bado, rudisha chemsha bongo zote na mazoezi ambazo umesahihisha.

Mwongozo wa Mwanafunzi

Mwongozo wa Mwanafunzi Haujajumuishwa kwenye hati hii,
lakini unapatikana katika hati tofauti.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Mwanafunzi.

Mwongozo wa Somo

Haukujumuishwa kwenye hati hii, lakini unapatikana katika hati tofauti.

.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Somo.

Mtihani

Majibu ya mtihani

Cheti cha Somo

Tazama ukurasa wa 5 wa mwongozo huu kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya mtihani na cheti.

Jina_____ **Kuitazama Biblia Kwa Haraka**

Tarehe_____ **Mtihani Toleo La 5**

Darasa_____ _____**Gredi**

Maswali Ya Kweli au Si Kweli (Alama 1 unusu kwa kila moja)

Maelekezo: Weka alama ya ___X____ ikiwa jibu ni kweli.

Weka alama ya ___O____ ikiwa jibu si kweli.

1. _____Katika Biblia kuna kupingana kiasi fulani.
2. _____Vitabu vyote vya Biblia viliandikwa na watu watano tu.
3. _____Kwa mara ya kwanza, Agano Jipya liliandikwa kwa lugha ya Kilatini, ili Wakristo peke yao waweze kulielewa.
4. _____Baadhi ya vitabu vya Biblia viliandikwa na watu ambao hawakuwa wanamtumikia wala kumwamini Mungu.
5. _____Kitabu cha kwanza kuandikwa katika Agano la Kale ni Mwanzo.
6. _____Ilichukua miaka kama 500 kwa vitabu vyote vya Biblia kuandikwa.
7. _____Baadhi ya vitabu vya Agano Jipya viliandikwa kabla Yesu hajafa.
8. _____Vitabu vyote vya Biblia, hapo kwanza, viliandikwa kwa mkono.
9. _____Unapojifunza mstari wowote katika Biblia, ni vizuri ujaribu kupata habari nzima inayohusiana na mstari huo.
10. _____Yesu peke yake ndiye aliyeunganisha vitabu vyote katika Agano la Kale.
11. _____Baadhi ya vitabu katika Biblia havijavuviwa na Mungu.
12. _____Yesu aliwaambia wanafunzi maneno yote ya kuandika kama yalivyo katika Agano Jipya.
13. _____Wakati waandishi wa vitabu vya Biblia walipokuwa wanaviandika, Mungu alikuwa anasogeza mikono yao ili wasifanye makosa yoyote.
14. _____Kuna baadhi ya unabii toka kwa Mungu, katika Biblia, ambao umekuwa na makosa.
15. _____Yesu alituambia kwamba Biblia ni kweli.
16. _____Wanaakiolojia wametumia miaka mingi wakichimba na kujifunza kuhusu miji ya kale iliyokuwepo wakati Biblia ilipoandikwa.
17. _____Magombo ya Dead Sea ni nakala ya baadhi ya vitabu vya Agano la Kale.

Maswali Ya Kweli au Si Kweli (yanaendelea)

18. _____Sheria nyingi za kitabibu katika Biblia zina madhara makubwa sana kwa afya yako.

19. _____Wakristo wa leo hawapaswi kuhangaika kusoma Agano la Kale kwa sababu liliandikwa kwa ajili ya Wayahudi, kabla ya Yesu kuja duniani.

20. _____Mungu aliweka unabii katika Biblia ili Wakristo waweze kutabiri juu ya wakati ujao, kama wanajimu wa kisasa na wasomaviganja wanavyofanya.

21. _____Yawezekana Yesu alitenda dhambi kidogo alipokuwa mvulana mdogo.

22. _____Katika Agano la Kale hakuna miujiza iliyoandikwa humo.

Maswali Ya Kuchagua Majibu (Alama 2 kila moja)

Maelekezo: Chagua jibu lililobora kuliko mengine na uweke herufi yake kwenye mstari ulioko mbele ya swali husika.

1. _____Biblia iliandikwa na watu kama?

   A. 5

   B. 40

   C. 60

2. _____Je, ilichukua miaka mingapi kwa Biblia kuandikwa?

   A. 200

   B. 500

   C. 1000

   D. 1500

3. _____Je, Paulo aliandika vitabu vingapi katika Biblia?

   A. 13

   B. 10

   C. 5

   D. Hakuandika hata kimoja

4. _____Mungu anataka mimi nipime mafundisho ya Biblia wakati gani, kwa kuyatendea kazi maishani mwangu?

   A. Hataki kabisa

   B. Mara moja moja

   C. Wakati wote

   D. Jumapili tu

5. _____Wakristo wasome Agano la Kale wakati gani?

   A. Wasisome kamwe

   B. Baada ya kuwa wamesoma Agano Jipya mara 5

   C. Mara moja moja

Maswali Ya Majibu Mafupi

1. Kuna vitabu:_____ katika Biblia. (alama1)

   Kuna vitabu _____ katika Agano La Kale. (alama1)

   Kuna vitabu _____ katika Agano Jipya. (alama 1)

2. Je, Agano la Kale liliandikwa katika lugha gani?_____
   (alama 3)

3. Agano Jipya liliandikwa katika lugha gani?_____
   (alama 3)

4. Kiasi cha watu _____ waliandika vitabu vya Biblia. (alama 3)

5. Ni nani mhusika muhimu kuliko wote katika Biblia?_____
   (alama 4)

6. Ni nini tukio muhimu kuliko matukio yote katika Biblia? (alama 4)

   _____

   _____

7. Eleza maana ya neno "kuvuviwa" linapotumika hivi: "Biblia *imevuviwa* na Mungu."
   (alama 6)

   _____

   _____

   _____

   _____

8. Ni zipi sababu kuu mbili za Mungu kuweka unabii katika Biblia?
   (alama 6, kila sehemu ina alama 3)

   1._____

   2._____

9. **Ni nini ushauri wako?** Doni si Mkristo. Anakuuliza swali: "Wewe unajuaje kwamba Biblia ni sahihi (yaani, ni ya ukweli)?"

   Andika mambo manne ambayo ungeweza kumwambia kuthibitisha kwamba Biblia ni sahihi. (alama 8, yaani 2 kwa kila sehemu)

   1. _____

      _____

   2. _____

      _____

   3. _____

      _____

   4. _____

      _____

10. Andika hapo chini majina ya **sehemu (au migao)** pamoja na **vitabu** vya Agano Jipya. (alama 17, yaani nusu alama kwa kila sehemu)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Kuitazama Biblia Kwa Haraka
Mtihani Toleo La 5
Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

Ukurasa Wa 1
Maswali Ya Kweli au Si Kweli
(Kila swali lina alama 1 na nusu)

1. 0 Si Kweli
2. 0 Si Kweli
3. 0 Si Kweli
4. 0 Si Kweli
5. 0 Si Kweli
6. 0 Si Kweli
7. 0 Si Kweli
8. X Kweli
9. X Kweli
10. 0 Si Kweli
11. 0 Si Kweli
12. 0 Si Kweli
13. 0 Si Kweli
14. 0 Si Kweli
15. X Kweli
16. X Kweli
17. X Kweli

Ukurasa Wa 2

18. 0 Si Kweli
19. 0 Si Kweli
20. 0 Si Kweli
21. 0 Si Kweli
22. 0 Si Kweli

Maswali Ya Kuchagua Majibu
(Kila swali lina alama 2)

1. B
2. D
3. A
4. C

Ukurasa Wa 3

5. C

Maswali Ya Majibu Mafupi

1. Alama 3 (alama moja moja)
   Biblia ina vitabu 66
   Agano la Kale lina vitabu 39
   Agano Jipya lina vitabu 27
2. Alama 3 – Kiebrania
3. Alama 3 – Kiyunani
4. Alama 3 – 40
5. Alama 4 – Yesu Kristo

Kuitazama Biblia Kwa Haraka
Mtihani Toleo La 5
Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

Ukurasa Wa 3 *(unaendelea)*

6. Alama 4
   Kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo.

7. Alama 6 (jibu linalopendekezwa)
   Roho Mtakatifu aliongoza mawazo ya watu. Hivyo, waliandika yale Mungu aliyotaka waandike.

8. Alama 6 (kila moja alama 3)
   Yanatakiwa majibu 2 tu.
   (Majibu yanayopendekezwa)
   - Kuthibitisha usahihi wa Biblia.
   - Kuwapa Wakristo tumaini.
   - Kuwahamasisha watu wamkaribie Mungu.
   - Isitumiwe kubashiri wakati ujao.

Ukurasa Wa 4

9. Alama 8 (2 kwa kila sehemu)
   (Majibu yanayopendekezwa)
   (Yanatakiwa majibu 4 tu)
   1) Unabii wote ndani yake umekuwa wa kweli na sahihi kabisa.
   2) Biblia inasema ni Neno la Mungu.
   3) Yesu alisema Biblia ni Neno la Mungu.
   4) Katika Biblia hakuna kupingana.
   5) Akiolojia inathibitisha kwamba Biblia ni sahihi.
   6) Taratibu za kimatibabu katika Biblia zinaithibitisha kwamba ni sahihi.
   7) Wewe mwenyewe jithibitishie kwamba Biblia ni ya kweli kwa kupima mafundisho yake katika maisha yako.

10. Alama 17 (nusu alama kwa kila sehemu).
    Tazama ukurasa wa 17 wa *Mwongozo Wa Mwanafunzi* ili upate orodha ya vitabu vya Agano Jipya na migawanyo yake.

Hongera

_____

Amemaliza

Kuitazama Biblia Kwa Haraka

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya
na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio utaendelea
na masomo yako yajayo.

Wakufunzi _____

Tarehe _____

Hongera

_____

Amemaliza

Kuitazama Biblia Kwa Haraka

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya
na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio utaendelea
na masomo yako yajayo.

Wakufunzi _____

Tarehe _____